
POLISI RAFIKI






POLISI
RAFIKI
Afande, upo kundi lipi?

Waandishi: Godfrey Telli, Vic Missiaen (Padri) na Mariam Kessy
Wachangiaji: Paul Ruzoka (Askofu) na Laurian Tibasana (Kamishna wa Polisi)
Katuni: Marco Tibasima
Mhariri: Rakesh Rajani

Kimeandaliwa na:

© HakiElimu 2005
SLP 79401, Dar es Salaam, Tanzania
info@hakielimu.org

© Tume ya Haki na Amani - TEC 2005
SLP 2133, Dar es Salaam, Tanzania
tec@cats-net.com

Kwa kushirikiana na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
SLP 75254, Dar es Salaam, Tanzania
lhrc@humanrights.or.tz

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi
Jeshi la Polisi Makao Makuu
SLP 9492, Dar es Salaam, Tanzania

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijiabu hiki kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala mbili kwa kila mchapishaji.

ISBN 9987-423-08-6

Dibaji

Jeshi la Polisi nchini Tanzania limeendelea kuwa moja ya vyombo vya dola vinavyofanya kazi kwa ukaribu na kwa ushirikiano na wananchi.

Kazi kubwa ya Polisi ni kuwalinda wananchi na mali zao. Yaani kusimamia hali ya amani, utulivu na usalama nchini. Kamwe polisi hawawezi kufanikiwa kutekeleza kazi hizi bila kushirikiana na raia. Kwa maana nyingine polisi hutekeleza wajibu wao kwa ridhaa ya wananchi.

Nafasi na wajibu wa raia katika kusaidia polisi ni muhimu ujengwe katika uhusiano mwema: uhusiano wa kidugu na wa kuaminiana. Polisi hawapaswi kuogopwa. Ni watumishi wa karibu wa wananchi; ni rafiki wa raia.

Kijitabu hiki kinalenga kuwakumbusha raia tangu wale wenye umri mdogo, kuwaona polisi kama watu wa karibu nasi na tunaopaswa kushirikiana nao. Lengo kuu la kijitabu hiki ni kubadili mtizamo wa jamii, tangu umri mdogo kuhusu Jeshi la Polisi.

Kwa upande mwingine, Polisi wanatakiwa kutambua wajibu wao wa kuwa wema, watulivu na wavumilivu kwa watu katika kutekeleza kazi zao. Ni kwa njia hiyo peke yake Polisi wataweza kujijengea mazingira ya kirafiki, ya ushirikiano na wananchi na ya kutoogopwa. Ni lazima wawe watu wa kuheshimu na kulinda haki za bindamu na wenye moyo wa huruma hasa kwa wale wanaowakimbilia kuomba msaada wao.

Ninatumaini kijitabu hiki kitasaidia sana watoto na raia wote wanapopata matatizo waweze kuwakimbilia polisi badala ya kuwakimbia. Kitasaidia pia kuwakumbusha Polisi kuwa ni watumishi wa raia na kwa hivyo ni lazima wawe na upendo kwa raia.

Ombi langu kwenu nyote ni kwamba ukimuona polisi anaitendea jamii jambo jema tuarifu ili atambuliwe kuwa ni mtimizaji wa wajibu wake na ni mfano mzuri kwa wenzake; na kama anatenda mambo kinyume cha maadili ya kazi yake tuarifu pia ili aweze kusahihishwa.

Kijitabu hiki ni mchango muhimu katika elimu kwa wananchi na hasa wale wenye umri mdogo. Aidha kijitabu hiki ni changamoto kwa taasisi na asasi nyingine zenye uwezo wa kufanya hivyo; kuiga mfano huu. Kwa ajili hiyo ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Tume ya Haki na Amani ya Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), HakiElimu na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa kuandaa kijitabu hiki.

Wapendwa watoto, polisi na raia wote kwa ujumla, mnakaribishwa kusoma kijitabu hiki kwa furaha na utulivu ili mpate kukielewa vyema; na kuishi kutokana na mafunzo mliyoyapata.

Nawatakieni usomaji mwema!

Omar Iddi Mahita,
Inspekta Jenerali wa Polisi,
Juni 2005

Utangulizi

Kijitabu hiki ni mwongozo rahisi wenye kuainisha majukumu na uhusiano baini ya Jeshi la Polisi na wananchi kwa ujumla. Uhusiano ambao kimtazamo wengi hawakuufahamu; kwani katika maisha ya kawaida malezi yatolewayo kwa watoto ni kuwaogopa Polisi.

Wengi walidhani ni vyema Polisi ajenge uadui na raia ili aweze kufanya kazi yake kwa ufanisi. Nia ya kijitabu hiki ni kuwajengea watoto na jamii yote fikra ya kuwaona Polisi kama rafiki wa kweli. Ni muhimu kwa jamii kushirikiana wote kujenga fikra hiyo.

Jeshi la Polisi ni mlinzi wa amani na maelewano. Huu ni wajibu mkubwa kwa jamii na Polisi. Kuzingatia sheria na taratibu tu haitoshi, bali pia kujenga uhusiano na ushirikiano mwema na Jeshi la Polisi. Huu ni wajibu wa kila mtu; watoto, Polisi na raia wote kwa ujumla.

Ninayo furaha kuwa kazi ya kutayarisha kijitabu hiki imekamilika. Ninamshukuru Inspekta Jenerali wa Polisi, Omar Iddi Mahita, kwa kuandika dibaji ya kijitabu hiki. Nawashukuru sana HakiElimu kwa kushiriki kuandika kijitabu hiki na kugharamia uchapishaji. Nawashukuru pia Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa mchango wao wa mawazo.

Kwenu watoto, Polisi na raia wote kwa ujumla tunawaletea kijitabu hiki mkisome kwa furaha na utulivu mkubwa ili kitujengee urafiki baina yetu sote kwa manufaa ya amani ya Taifa letu.

Nawatakia maisha yenye furaha, amani na upendo.

Askofu Paul Ruzoka
Askofu wa Jimbo la Kigoma na
Mwenyekiti wa Tume ya Haki na Amani - TEC
Juni 2005


POLISI RAFIKI YUPO KWA AJILI YA KUKULINDA WEWE




POLISI BORA WANAFANYA KAZI KWA UPENDO NA KUFUATA HAKI ZA BINADAMU.
NDIO KABULA, POLISI BORA WAPO HAPA KUTULINDA NA SI KUTUPIGA. TUNAPASWA KUJISIKIA AMANI POLISI WANAPOONEKANA MITAANI!

POLISI RAFIKI HAPOKEI RUSHWA




MIMI NAONA ANAMTAHADHARISHA DEREVA AREKEBISHE GARI LAKE ILI KUEPUKA AJALI!
POLISI BORA KAMWE HAWACHUKUI RUSHWA!
NDIO, ANAJUA KWAMBA DEREVA ANAHITAJI FEDHA ILI AKAREKEBISHE GARI LAKE!
MITUMBA
TIZED1

POLISI RAFIKI ANAWASAIDIA WATOTO





KWANI YULE POLISI YUPO HAPA KWA SABABU GANI-SIO KUTUSAIDIA?
NDIO! TAZAMA ANAMSAIDIA YULE MTOTO KUVUKA BARABARA! POLISI BORA ANASIMAMISHA MAGARI KWANZA ILI KUHAKIKISHA WATOTO, WALEMAVU NA WAZEE WANAVUKA BARABARA KWA USALAMA.
VITA
MJINI


POLISI RAFIKI ANAWASAIDIA WATU KUSHIRIKI KATIKA MASUALA YA KISIASA
HE! NA SISI TUJIUNGE NA MAANDAMANO JAMANI!
USIWE MJINGA WEWE! UKITAKA KUJUA POLISI WANAPIGAJE WATU KWA VIRUNGU HADI KUWATIA NGEU JARIBU KUANDAMANA, UTAKULA KIPIGO CHA PAKA MWIZI!
MISAADA ZAIDI KWA WALEMAVU
TUNASIMAMIA HAKI ZETU!
SISI NI BINADAMU PIA!
Misaada zaidi Kwa WASIOONA!


LAKINI UHURU WA MIKUSANYIKO NA MAANDAMANO NI HAKI YETU KI-KATIBA.
POLISI BORA KAZI YAO NI KUHAKIKISHA MAANDAMANO YANAKUWA NI YA AMANI
Misaada zaidi kwa WALEMAVU!
SISI NI BINADAMU PIA
Tunastahiki Kuheshi

POLISI RAFIKI WANASIMAMIA UTULIVU MITAANI




UNAONA? POLISI AMEFANYA USHUJAA KUMWOKOA. POLISI BORA WANAJALI NA KULINDA UHAI WA KILA MTU!
marcowocka@yahoo.com


POLISI RAFIKI ANAWASAIDIA WAZEE NA WASIOJIWEZA




MAMA WEE! HUWEZI KUAMINI... NI KWELI KABISA ANAWASAIDIA KUINGIA KWENYE BASI. AJABU HII!
BASI

POLISI RAFIKI WANAFANYA UCHUNGUZI KWA HAKI




NA UKIZUBAA TU ANAKUPIGA BUTI!
HAPANA! POLISI WANAFANYA UPELELEZI TU; WANAMTENDEA YULE MTU NA FAMILIA YAKE KWA HESHIMA!
WANAJARIBU TU KUHAKIKISHA MAZINGIRA YOTE HAPA MTAANI NI SALAMA! HUENDA IKAWA MTU YULE ANASHUKIWA KUFANYA KITU KIBAYA SANA!

POLISI RAFIKI ANAWASALIMU WATU WOTE NA KUWATENDEA KWA HESHIMA




NZURI! HAMJAMBO?
AHAA! KUMBE WANAONEKANA WAKO POA SANA HAWA POLISI!
HATUJAMBO!
DUKA

POLISI RAFIKI ANAWAOKOA WATU WASIUMIZANE




POLISI SAIDIAA!
RAFIKI YETU
ANASHAMBULIWA!

POLISI RAFIKI ANAWATIA WATU NGUVUNI PALE TU WANAPOVUNJA SHERIA




UMEONA? POLISI BORA NI RAFIKI ZETU!
WAKO HAPA KUTULINDA NA HATARI!
HIVYO TUNAWEZA KUISHI KWA AMANI !

Kijitabu hiki ni mwongozo rahisi wenye kuainisha majukumu na uhusiano baini ya Jeshi la Polisi na wananchi kwa ujumla. Uhusiano ambao kimtazamo wengi hawakuufahamu; kwani katika maisha ya kawaida malezi yatolewayo kwa watoto ni kuwaogopa Polisi.

Wengi walidhani ni vyema Polisi ajenge uadui na raia ili aweze kufanya kazi yake kwa ufanisi. Nia ya kijitabu hiki ni kuwajengea watoto na jamii yote fikra ya kuwaona Polisi kama rafiki wa kweli. Ni muhimu kwa jamii kushirikiana wote kujenga fikra hiyo.

Jeshi la Polisi ni mlinzi wa amani na maelewano. Huu ni wajibu mkubwa kwa jamii na Polisi. Kuzingatia sheria na taratibu tu haitoshi, bali pia kujenga uhusiano na ushirikiano mwema na Jeshi la Polisi. Huu ni wajibu wa kila mtu: watoto, polisi na raia wote kwa ujumla



HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa ubora haki za binadamu na demokrasia katika elimu na jamii. Tunafanya hivyo kwa kuwezesha jamii kupata habari kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera; kuchochea ubunifu wa mijadala ya umma; kufanya utafiti yakinifu uchambuzi wa sera na utetezi na kushirikiana na wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Barabara ya Mathuradas 739 • Upanga
SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org
Simu: (255 22) 2151852 au 3 • Fax: 2152449

Tume ya Haki na Amani ya Baraza la Maaskofu Tanzania ni kitengo cha kanisa katoliki Tanzania. Tume inawajibika kuhamasisha watu waelewe haki zao na kuzitetea. Pia inafanya kazi ya kufundisha watu kutimiza wajibu wao kwa ajili ya maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Tume ya Haki na Amani – TEC
SLP 2133, Dar es Salaam, Tanzania
tec@cats-net.com